**Mwongozo p1**

1. Lazima sura ya insha hii ibainike wazi.
    - Atumie nafsi ya kwanza
    - Ajihusishe la si hivyo hatakuwa amejibu swali kwa hivyo atuzwe D ya alama 3.
    - Aseme ni mahojiano baina ya nani na nani kama anwani na apigie mstari.

**Azingatie maudhui kwa mfano**

- Ukosefu wa chakula cha kutosha
- Barabara mbovu – hazipitiki
- Ukosefu wa vyombo vya kusafirisha k.v. magari
- Ukosefu wa usalama
- Uhasama baina ya makabila / koo za sehemu husika
- Wizi wa chakula kutoka vyombo vya dola n.k
- Hamahama za watu
- Uchochezi toka kwa wanasiasa
- Idadi kubwa ya wanaotegemea msaada huu
- Kuharibika kwa chakula hiki
- Athari ya hali ya anga.
- Ukosefu wa mahali pa kuhifadhia.

  * Hakiki hoja zingine

**N/B** Maudhui angalau sita na zifafanuliwe vizuri

2.
    - Serikali kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana nchini kote nchini
    - Kuimarisha huduma za usafiri m.f kuboresha barabara
    - Kuwashawishi raia kutembelea vivutio mbalimbali nchini
    - Kupugnuza ada za kiingilio kwenye vivutio hivi
    - Kujengwa kwa hoteli za kisasa katika maeneo yanayopendelewa Zaidi na watalii.
    - Kurahisisha shughuli ya kupata kibali cha kuwa nchini.
    - Kuviboresha vivutio hivi vya utalii k.m tamaduni
    - Kuboresha huduma katika angatua (airport) na bandari zetu ili kuwapa watalii mapokezi yafaayo

- Kutoa ulinzi kwa wanyama pori walio na hatari za kuangamizwa na majangili
- Kuhakikisha waelekezi wa watalii wanapata mafunzo mwafaka hasa kuhusiana na mlahakama vyema
- Kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana kwenye vivutio na kwa ada ya chini k.m intaneti, benki n.k

**Zozote tano zifafanuliwe vizuri**

3. **Maana** ya methali hii ni kuwa mtu anayechibuka ngozi akilima hafi njaa

   **Matumizi:** Kuwahimiza watu wawe na uvumilivu wa kukabiliana na shida au jambo gumu kwa kuwa hatimaye wataishia kufaidika.

   - Si lazima matahiniwa aeleze maana ya ndani nan nje ya methali.
   - Mtahiniwa atunge kisa kimoja tu kinachoafikian na maana ya methali husika.
   - Pande zote mbili za methali zijitokeze wazi ( kuchanika – kujibidiisha / kuteseka na h atimaye kutokufa njaa – kufaidika) . Si lazima iwe nusu bin nusu lakini zionekane.
   - Asiposhughulikia pande zote mbili atakuwa amepungukiwa kimaudhui

4. Mtahiniwa aweza kuangazia yafuatayo

   - Shule yake ni mmoja wa zile zilizokoza matokeo
   - Baadhi ya wanafunzi shuleni mwake wakoza matokeo lakini / alibahatika kupata zake
   - Sababu ya matokeo kufutiliwa mbali ( wizi wa mtihani)
   - hatua mbalimbali alizochukua kukabiliana na tukio hili
   - Hatima ya tukio hili n.k.